

HALMASHAURI YA WILAYA YA NEWALA



FOMU YA KUJIUNGA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021.

SHULE YA SEKONDARI MAPUTI

S.L.P 227, NEWALA

Barua pepe: maputi445@gmail.com

Tarehe:

Kumb. Na.

Jina la Mwanafunzi: _____

1.0 UTANGULIZI

Hongera kwa kuchaguliwa kujiunga na masomo ya sekondari kidato cha kwanza 2020 katika Shule ya Sekondari Maputi. Shule ya sekondari Maputi ni Shule ya kutwa na ya mchanganyiko, ipo umbali wa kilometra 2 kutoka makao makuu ya halmashauri ya wilaya ya Newala.

Mhula wa kuanza masomo unaanza tarehe 11/01/2021, hivyo unatakiwa kuripoti Shulenii kuanzia tarehe 04.01.2021 kwa ajili ya usajili. Zoezi la usajili la usajili litafungwa ijamua tarehe 08.01.2021 saa 9:00 mchana.

1.1 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

A. Sare za shule kwa wavulana.

- i. Shati nyeupe mbili (2) za mikono mifupi za kitambaa cha pamba au tetron. Zisiwe zenye kuona(transparent), kubana wala pan asana.
- ii. Suruali mbili za rangi ya bluu bahari (dark blue) **ZITASHONWA SHULENI TU** kwa gharama za Tsh **20,500/=** Kwa suruali moja. Hivyo suruali mbili gharama zake ni Tsh 40,000/=
- iii. Viatu vya ngozi nyeusi jozi mbili (2). Mwanafunzi hataruhusiwa kuvaa viatu vya plastiki.
- iv. Soksi za rangi nyeusi jozi mbili (2)
- v. Bukta za michezo rangi ya bluu
- vi. Raba za michezo
- vii. T-shirt kwa ajili ya michezo rangi ya bluu
- viii. Sweta la mikono mirefu rangi ya kijani, livaliwe wakati wa baridi tu.
- ix. Track suit rangi nyeusi kwa ajili ya michezo
- x. Suruali rangi nyeusi zisizo bana. Zitavaliwa wakati shughuli za nje ya darasa
- xi. T-shirt za Shule (Second dress). Zinapatikana shuleni kwa Tsh 10,000/=

B. Sare za shule kwa wasichana.

- i. Shati nyeupe mbili (2) za mikono mifupi za kitambaa cha pamba au tetro. Zisiwe za kuona (transparent), kubana wala pan asana. Kwa wale wanaovaa Hijabu, inatakiwa iwe ya kushona kwa fundi na ifanane na shati nyeupe ya shule. Hijabu itashonwa shuleni tu.
- ii. Sketi mbili za rangi ya kijani. **ZITASHONWA SHULENI TU** kwa gharama ya Tsh **26,000/=** kwa sketi moja, hivyo mzazi utalazimika kulipia Tsh 52,000/= kwa sketi mbili.
- iii. Viatu vya ngozi nyeusi jozi mbili (2) visiwe na visigino virefu. Mwanafunzi hataruhusiwa kuvalaa viatu vya plastiki maarufu kama yebo yebo.
- iv. Soksi za rangi nyeupe jozi mbili (2)
- v. Raba za michezo
- vi. T-shirt kwa ajili ya michezo rangi ya bluu
- vii. Sweta la mikono mirefu rangi ya kijani, livaliwe wakati wa baridi tu.
- viii. Track suit rangi nyeusi kwa ajili ya michezo
- ix. Gauni la rangi ya maruni, litavaliwa wakati wa shughuli za nje ya darasa.
- x. T-shirt za Shule (Second dress). Zinapatikana shuleni kwa Tsh 10,000/=

1.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU.

Pamoja na sare za shule mambo mengine anayopaswa mzazi kumtekelezea mwanafunzi pindi anaporiti ni:-

- a) Vifaa vya darasani: Daftari kubwa (counter book) 11, Rimu 1 ya karatasi za A4 kwa ajili majoribio na mitihani, mkebe wa hesabu wenye vifaa vyote, kalamu za wino wa mweusi au bluu pamoja na kalamu ya makaa.
- b) Kumchangia chakula awapo shuleni

1.3 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu Na 25 ya mwaka 1978 pamoja na marekebisho yake ya sharia Na 10 ya mwaka 1995. Aidha, Shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Rais- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni.

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- ii. Mahudhurio mazuri na bidii katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima. Mzembe hatadumu hapa Shuleni.
- iii. Kuwahi katika kila shughuli za Shule na nydingine utakazopewa.
- iv. Kufahamu mipaka ya Shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote uwapo katika Shule hii.
- v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya Shule.
- vi. Kuvaa sare za Shule wakati wote uwapo Shuleni.
- vii. Kuzingatia sharia na kanuni za wakati wote.

1.4 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE AU KUSIMAMISHWA SHULE.

- i. Wizi.
- ii. Uasherati na ushoga
- iii. Ubakaji
- iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika.
- v. Kupigana au kupiga.
- vi. Kuharibu kwa makusudi mali za umma.
- vii. Kudharau bendera ya Taifa.
- viii. Kupata ujauzito au kusababisha ujazito
- ix. Kuoa au kuolewa.
- x. Kutoa mimba.
- xi. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga Amani na usalama wa Shule au watu.
- xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
- xiii. Kuwa na simu ya mkononi

1.5 NYARAKA MUHIMU ZA KUWASILISHA SHULENI SIKU YA KURIPOTI.

- i. Medical Examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
- ii. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makossa ya jinai.
- iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sharia, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na Shule.
- iv. Nakala ya cheti cha kuzaliwa au Affidavit.

Tafadhali soma kwa umakini maelekezo au maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI MAPUTI.

HAMIDU A. LIKULU (MKUU WA SHULE)

MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI NA MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO

MIMI.....	WA KIDATO CHA	SHULE YA
SEKONDARI.....		
NIMEZALIWA TAREHE.....	MWEZI.....	MWAKA.....
NIMEMALIZA DARASA LA SABA KATIKA SHULE YA MSINGI		
.....	MWAKA	
ANUANI YA NYUMBANI NI		
Nimesoma maelekezo na sharia zote za shule na kuzielewa na naahidi kuwa mwanafunzi bora mwenye bidi na utii muda wote. Naahidi pia sitashiriki katika migomo, fujo na makossa ya jinai niwapo ndani nan je ya shule.		
SAHIHI YA MWANAFUNZI.....		
JINA KAMILI LA MWANAFUNZI	TAREHE	

MZAZI KUKUBALIANA NA SHERIA NA MAELEZO YA SHULE

Mimi	mzazi/mlezi wa mwanafunzi
.....	ambaye anajiunga na shule ya sekondari Maputi kidato cha kwanza mwaka
	Naahidi kumpatia mahitaji yote anayotakiwa kufika nayo shulen i kama yalivyoandikwa katika barua hii. Pia nitahakikisha amesoma sharia za shule na kuzielewa ipasavyo. Nakiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.
SAHIHI.....	JINA LA MZAZI/MLEZI.....
NAMBA YA SIMU.....	

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO A STUDENT

PART "A"

THE HEADMASTER,
MAPUTI SECONDARY SCHOOL,
P. O BOX 227
NEWALA.

TO: THE MEDICAL A/C

.....
.....

Please examine Aged years as to his/her fitness for admission and pursue secondary education.

Signature:

Designation:

PART "B" (To be completed by a medical officer)

Please examine the following and comment

1. Blood count (red and white blood cells)
2. Stool
3. Urine analysis
4. Syphilis test
5. T.B
6. Ears
7. Eyes
8. Spleen
9. Blood pressure
10. Abdomen
11. Pregnancy
12. Any other (e.g physical disability, chronic diseases etc.)

PART "C" (To be completed by a medical officer)

MEDICAL CERTIFICATE

I have examined the above named student and recommend that he/she is physically fit/unfit for admission into secondary school.

Date:

Signature:

Hospital:

Designation:

AFFIDAVIT

I Of

Village district, Tanzania who have by make an oath and state as follows that I am the (father, mother, near relative) of who was born at On

That I was present at shortly after the birth of the said or that I had a personal direct knowledge of the birth of the said account of that the father/mother of were born in Tanzania and are citizen of Tanzania.

SIGNATURE OF DEPENDANT

SWORN AT

THIS

BEFORE ME

NAME

QUALIFICATION

SIGNATURE